Students Name: ...............................................................................

School Name................................................. Index Number ...............

**336/2**

**LUGHA NA FASIHI YA KISWAHILI**

KARATASI YA PILI

SAA MBILI

JULAI 2025

# HES MOCK EXAMINATIONS 2025

## UGANDA CERTIFICATE OF EDUCATION

LUGHA NA FASIHI YA KISWAHILI
KARATASI YA PILI

UFAHAMU NA UCHAMBUZI WA FASIHI

SAA MBILI

**MAAGIZO KWA WATAHINIWA:**

- Karatasi hii ina sehemu **mbili; A** na **B.**
- Mtahiniwa anapaswa kujibu maswali **yote**

**SEHEMU A : UFAHAMU**

**1. Soma habari ifuatayo kisha ujibu maswali.**

Kuishi nikupitia kwenye mitinani ya namna nyingi. Kuminyanana kufaulu katika jaribio lolote kunahitaji akili tulivu. Nao utulivu wa akili unatokana na kujiamini kunakovyazwa na matayarisho thabiti.

Mtahiniwa anawezaje kujiandaa ili aikabili mitihani vilivyo? Jambo la msingi katika kumchochea mwanafunzi ni kumfahamisha kuwa elimu ndiyo nguzo ya kutegemea maishani. Kwa hivyo, anaposoma, asisome kwa kufaulu mitihani tu, bali alenge hasa kuelimika. Mitihani ni thibitisho na kipimo cha kuhitimu viwango mbalimbali vya elimu.

Mtahiniwa asife moyo kwa kuuona muda uliobakia kabla ya mtihani kuwa mchache. Kama hakujisomea kwa bidii ilivyopasa katika siku zilizopita, si neno, yaliyopita si ndwele, ganga yajayo. Katika mwaka huu wa mwisho, sharti mtahiniwa aupe uzembe kisogo na kuuasi kabisa, kwani fanaka zipo mvunguni; na azitakaye, sharti ainame. Mwananfunzi asifanye ajizi katika kuzingatia masomo. Afahamu ya kuwa sasa bwana wa kutumikiwa ni mmoja – kisomo.

Masikio hayapiti kichwa. Mtahiniwa autakaye ufanisi, ayafuate mawaidha yote ya walimu wake na wale wote wenye ujuzi. Ushirikiano na wanafunzi wengine katika vikundi vikundi ni wa manufaa, kwani kidole kimoja hakivunji chawa.

Katika kufanya marudio ya binafsi, ni vyema kuwa na mpango maalum unaoonyesha jinsi kila saa na dakika ya kujitayarisha inavyotumiwa. Utaratibu huu, ulipe kila somo nafasi ya kutosha ya kufanyiwa marejeleo. Yale masomo yenye ugumu zaidi kwa mwanafunzi, yasisitizwe. Mpango huu hautakuwa na maana yoyote kama hautaheshimiwa kwa kuzingatiwa.

Mtahiniwa ajitahini kwa mazoezi mengi ya ziada kwa kutoa majibu kwa kuandikwa au kuzungumzwa. Ni vizuri kupitia mitihani iliyotangulia na majaribio mengine. Muda wa kujibu maswali mbalimbali unapaswa uwesambamba na ule uliowekewa maswali ya namna hiyo katika mtihani wenyewe. Hoja si kujibu maswali tu, bali ni kuyajibu vile yalivyoulizwa.

Ubongo wa mwanadamu haujai, na elimu nayo haina mipaka. Lichaya yale afunzwayo darasani, mtahiniwa ajiongezee elimu kwa usomaji mpana

unaofaa. Hali kadhalika, vyombo vya upashanaji habari na mawasiliano ni muhimu kwa kuelimisha na kuendeleza.

Hata hivyo, kila jambo lina kadiri yake. Kama vile mchana wa mwangaza unavyopishana na usiku wa giza, kazi na juhudi za mwanafunzi za kujiandaa sharti zipishane na mapumziko. Hiyo ni kanuni ya maumbile. Mwanafunzi ajipangie wakati na namna ya mapumziko. Katika wakati huu wa kupumzisha akili, aamue jinsi atakavyonyoosha viungo vya mwili. Anaweza kujistarehesha kwa gumzo la maana, matembezi, sinema au mchezo mzuri. Bongo pia, litafanya kazi barabara iwapo atakula chakula bora na kupata usingizi wa kutosha.

Je, kuhusu mtihani wa Kiswahili mwanafunzi ajiandae vipi?
Mtahiniwa hana njia ya mkatoila kujikakamua na kuijua lugha kwa upana na urefu wake. Kuijua lugha ni kuujua msamiati, kuufahamu muundo wake, na kuzitambua sheria zake. Ni lazima kuzijua semi na methali, maana na matumizi, kama zilivyobuniwa na wahenga. Itambidi mwanafunzi kumtegemea mwalimu wake, kupitia kumbukumbu za daftari zake na kusoma vitabu vyenye lugha sanifu. Mazoezi na mazoea ya uzungumzi wa lugha sanifu yana manufaa sana. Katika kiwango hiki, sharti mtahiniwa awe na akili tambuzi ya kuufahamu upeo wake wa lugha na kuutambua udhaifu wake. Mwanafunzi anapaswa kuwa macho ili akwepe athari za lugha za kimama na lugha zingine za kigeni mathalani, Kiingereza.

Swali la insha humpa mtahiniwa uwanja na uhuru wa kuonyesha ubingwa wake wa lugha. Kwa kujiandaa vema kwa swali hili, mtahiniwa angejibidiisha na kuandika mitungo mingi na ya aina mbalimbali. Insha hizi zote zifanyiwe marekebisho na masahihisho kufuatia maelekezo ya mwalimu. Mtahiniwa ajifunze zaidi kwa kuzisoma insha za wanafunzi wenziwe na hata ikiwezekana za wanafunzi wa shule zingine. Haya yote yatamwezesha mwananfuzi kuzijua aina za miundo na mitindo tofauti tofauti. Ajue pia ya kwamba kusoma vitabu vya miongozo ya uandishi wa insha ni muhimu sana.

Katika kuandika insha, kwanza, ni muhimu kuzingatia maagizo ya urefu utakikanao na jambo litakiwalo kuelezwa. Kama inapasa kufanya uchaguzi wa anuawani moja kati ya baadhi yazo, mtahiniwa afanye

busara ya kuchagua kichwa ambacho hana shaka nacho. Ikiwezekana kiwe kinalingana na mazingira na malezi anayoyafahamu. Mtahiniwa aisome tena na tena ile anwani aliyoiteua ili awe na uhakika wa lile hasa atakiwalo kuliandika.

Kuitayarisha insha kabla ya kuanza kuiandika ni jambo muhimu. Mtahiniwa ajue namna ata- kavyoianza insha yake, atakavyoiendeleza na jinsi atakavyoimaliza. Moja ya njia za kutayarisha insha ni kuandika vidokezo kadhaa. Vidokezo hivi hupatikana kwa kujiuliza maswali kama:
Nani?Lini?Wapi?Vipi?Kwa nini?
Mtahiniwa anapoandika, aandike habari za kuaminika, kuvutia na kusisimua. Insha iwe na mawazo mazito yaonyeshayo <u>ukomavu wa akili</u>. Msamiati unaotumiwa ulingane na kichwa. Mtungo uwe na mtiririko na mpangilio mzuri unaotenga mawazo katika aya tofauti. Usanifu wa lugha na unadhifu wa hati uzingatiwe tangu mwanzo hadi mwisho. Kwa kila hali mtahiniwa ajielezena aeleweke.

Aina mbalimbali za mitungo ziandikwe ipasavyo. Ikiwa ni barua, yazingatiwe masharti yake, hotuba ifuate utaratibu wa hotuba na kama ni kumbukumbu ifuate urasimu wa kumbukumbu. Matumizi <u>mwafaka</u>ya nahau, semi na methali yataupamba mtungo na kuupa mvuto kwa yeyote ausomaye. Ni vizuri kuipitia insha baada ya kuiandika, ili kuondoa makosa ya tahajia yawezayo kutokea wakati wa kuandika.
Ukweli ni kwamba, mwanafunzi yeyote atakuwa na <u>tashwishi</u> kidogo anapoukabili mtihani. Lakini, mwanafunzi ajiandaaye barabara hatakuwa na wasiwasi wa kumwondolea maarifa siku za mtihani zitakapowadia.

**Maswali**
a) Kufaulu mtihani kunategemea jambo gani hasa?
b) Kwa mujibu wa taarifa, mtihani una umuhimu gani?
c) Mtahiniwa anapaswa kufanya nini ili kuhakikisha kuwa amekamilisha mafunzo ya kuumudu mtihani?
d) Taja mambo matano muhimu ya kuzingatiwa katika uandishi wa insha.
e) Kigezo cha kuupima ujuzi wa mwanafunzi katika mtihani wa Kiswahili ni kipi?

SEHEMU B: **UCHAMBUZI WA FASIHI**

2. Soma dondoo hili kisha ujibu maswali yanaofuata.

| | |
|---|---|
| Bw. Naona: | Mimi ninaona kwamba mengi mabaya na ya harati yanatokea mheshimiwa kiongozi mkuu |
| Bw. Binafsi: | Mabaya kama yepi ambayo mimi sijaambiwa? |
| Bw. Naona: | Mimi ninaona watu wameanza kuamka mheshimiwa kiongozi mkuu |
| Bw. Binafsi: | Kwani watu wangu walikuwa wamelala siku zote hizi? |
| Bw. Naona: | ndivyo. Watu wako wanavyosema sasa, ingawa mimi naelewa kwamba chini ya uongozi wako wameamshwa kwa mengi. Kwa hivyo wanapaswa wawe macho mheshimiwa kiongozi mkuu. |
| Bw. Binafsi: | Unasemaje ofisa? |
| Bw. Salimina: | Wao ndivyo wanavyokazania kuwa wanapaswa wawe macho kwani wanahisi wamella au wamelazwa mheshimiwa kiongozi mkuu |
| Bw. Binafsi: | Elimu yote hii niliyoisambaza nchini bado wao wana hisi wamelala? |
| Bw. Salimina: | Wao wanasema kwamba elimu yenyewe inayotolewa ni elimu uhange. Ni elimu inayo……. inayo………..inayotukuza….aaa…. |
| Bw. Binafsi: | Sema tu. Mimi nataka kujua ukweli. |
| Bw. Salimina: | Inayotukuza uongozi wako badala ya kukuza taifa lenyewe ambalo wao wanaliona si taifa. |
| Bw. Binafsi: | Si taifa? (Sasa waziwazi amekasirika) Taifa hili linalojulikana vizuri duniani kote si taifa? Taifa linaloendeshwa kwa usalama si taifa? Taifa ambalo watu wake wanatibiwa wakiumwa sitaifa? Taifa ambalo watu wake hawasemi ovyo ovyo si taifa? Kama hili si taifa basi lipi taifa?” |

***Maswali***

*(a)* Chambua mandhari ya onyesho huu.
*(b)* Jadili ujumbe unaojitokeza katika dondoo hili .
(c) Fafanua mbinu za lugha zinazojitokeza katika dondoo hili.
(d) Unapata hisia zipi baada ya kusoma dondoo hili. Eleza
(e) Eleza maadili unaopata baada ya kusoma dondoo hili.